# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA

# MKATABA WA MAKUBALIANO KATI YA HALMSHAURI YA KIJIJI CHA MAGWAMILA NA SONGEA SUKARI LIMITED KWA AJILI YA KILIMO CHA MIWA NA UJENZI WA KIWANDA CHA KUZALISHA SUKARI.

KATI YA

HALMASHAURI YA KIJIJI CHA MAGWAMILA

NA

SONGEA SUKARI LIMITED.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA**

Tel:025-2602320/2602176
Fax:025-2602320/2602176
Email :ded@songeadc.go.tz,

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Songea,
barabara ya Halmashauri,
S. L. P 995
**57183 SONGEA, RUVUMA**

# MKATABA WA MAKUBALIANO KATI YA HALMASHAURI YA KIJIJI CHA MAGWAMILA NA SONGEA SUKARI LIMITED KWA AJILI YA KILIMO CHA MIWA NA UJENZI WA KIWANDA CHA KUZALISHA SUKARI.

Mkataba huu wa makubaliano umefanyika leo tarehe 23 Mwezi 01 Mwaka 2024.

**KATI YA**

**Halmashauri ya Kijiji cha Magwamila**, ni kijiji kilichopo katika mamlaka ya Serikali za Mitaa, ambayo ilianzishwa kwa kifungu cha sheria na. 287 R.E 2002, yenye anwani S.L.P. 995 Songea, kwa anwani ya kudumu yenye ofisi zilizopo Kijijini Magwamila, Kata ya Muhukuru Lilahi, katika Wilaya ya Songea, Mkoani Ruvuma – Tanzania, ambaye katika Makubaliano haya atajulikana kama **''Mwenye ardhi''** kwa upande mmoja.

**NA**

**SONGEA SUKARI LIMITED,** ni kampuni iliyosajiliwa Tanzania yenye anwani S.L.P. 2924 Dar es Salaam na kupewa cheti cha **usajili na. 158658550 kilichotolewa tarehe 31 oktoba, 2022** na Msajili wa Makampuni Tanzania (BRELA), Kampuni hii imeanzishwa mahsusi kwa ajili ya kutekeleza mradi mkubwa wa kilimo cha miwa na ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha sukari kijijini Magwamila. Ambaye katika Makubaliano haya atajulikana kama **''Mwekezaji''** kwa upande mwingine.



KSH

## 1. TAFSIRI

Katika mkataba huu wa makubaliano, kutakuwa na vifupisho vya baadhi maneno yenye maana kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **MM** | Mkataba wa Makubaliano |
| **PANDE** | Magwamila Village Council na Songea Sukari limited |
| **KLPD** | Kilolita kwa siku |
| **TCD** | Kusagwa Tani kwa Siku |
| **MWEKEZAJI** | Songea Sukari limited |

## 2. MADHUMUNI YA MKATABA HUU WA MAKUBALIANO

Madhumuni ya Mkataba huu wa Makubaliano ni kuleta uhusiano wa uwekezaji baina ya Halmashauri ya Kijiji cha Magwamila na kampuni ya uzalishaji wa Sukari ya Songea Sukari Limited.

## 3. UWIANO WA MRADI

Mkataba huu wa Makubaliano kati ya pande hizi mbili utakuwa na uwiano kama ifuatavyo;

### 3.1 Uletaji wa ajira

Mradi huu unategemewa kuzalisha ajira. kwa kiasi cha watu elfu tano(5,000) mpaka elfu sita (6,000) za moja kwa moja, ambazo kipaumbele kitakua kwa Wakazi wa Kijiji cha Magwamila. Ajira zisizo za moja kwa moja zitapatikana pindi uzalishaji utakapoanza.

### 3.2 Wazalishaji wa nje

Katika kipindi chote cha uwekezaji, utaanzishwa mpango wa wazalishaji wa nje (Out Growers) ambapo kampuni itatoa utaalamu na elimu ya kulima miwa, mbegu na huduma nyinginezo kwa wakulima wa miwa ambao watakuwa na mkataba wa kuuza miwa kwa kampuni ya Songea Sukari Limited. Wanakijiji wanaozunguka watakuwa na fursa ya kulima miwa na kumuuzia Mwekezaji moja kwa moja.



12 SHA

## 4. MAJUKUMU YA KAMPUNI KATIKA JAMII.

**4.1** Mwekezaji atalipa tozo kwa Halmashauri ya kijiji cha Magwamila na Halmashauri ya Wilaya ya Songea zilizopo kwa mujibu wa sheria.

**4.2** Mwekezaji atalipa fidia kwa wanakijiji wazawa ambao wamekua na maeneo yao ya kilimo katika eneo la uwekezaji. Wanakijiji hao ni wale waanaotambuliwa serikali.

**4.3** Mwekezaji atachangia kutoa Huduma mbalimbali za maendeleo kwa Kijiji cha Magwamila na vijiji jirani vinavyozunguka mradi huo, Mathalani kuchangia katika Huduma za kijamii.

**4.4** Mwekezaji atachangia upatikanaji wa umeme kijijini Magwamila na vijiji jirani, umeme ambao utaunganishwa na grid ya taifa.

**4.5** Mwekezaji atachangia upatikanaji wa sukari kijijini Magwamila na nchini kwa ujumla, ambapo kiasi cha sukari tani 79,200 kinatarajiwa kuzalishwa kwa mwaka katika awamu ya kwanza hadi kufikia kiasi cha tani118,000 kinatarajiwa kuzalishwa kwa mwaka katika awamu ya pili.

**4.6** Uwekezaji huo pia utazalisha Ethanol takibani lita 8,000,000 kwa mwaka katika awamu ya pili (2) ya mradi.

## 5.0 MPANGO WA USHIRIKIANO

### Kwa ujumla

**5.1** Halmashauri ya Kijiji cha Magwamila inamkaribisha Mwekezaji Songea Sukari Limited kuzalisha sukari, umeme na ethanol kwenye kijiji cha Magwamila, kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Mkoa wa Ruvuma –Tanzania.

**5.2** Mradi wote utafanyika kijijini Magwamila katika kata ya Muhukuru Lilahi na Kijiji cha Nakawale Kata ya Muhukuru.

## 6.0 MAJUKUMU YA KILA PANDE

### 6.1 Halmashauri ya Kijiji cha Magwamila.

Halmashauri ya Kijiji cha Magwamila, watatoa ardhi yenye ukubwa wa hekta 30,000 Kijiji ambacho kinahusika na mkataba huu. Hatimiliki ya Shamba itamilikishwa kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania na mwekezaji atapewa Hatimiliki isiyokuwa ya asili (Derivative Rights).



K SAH

Hekta 14,000 zitapatikana katika kijiji cha Nakawale katika Halmshauri ya wilaya ya Songea,ardhi hii itakua kwaajili ya wakulima wa nje (out growers) Umilikaji wa shamba hili pia utakuwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea na Mwekezaji atakapohitaji kupanua uwekezaji wake miaka ijayo atalazimika kuomba kwa kufuata sheria na taratibu za wakati huo.

**6.2 Songea Sukari Limited**

Mradi wote ulioelezwa unahitaji eneo lenye ukubwa wa 44,000 Hekta kwa awamu mbili za utekelezaji. Songea Sukari Limited kwa upande wake watachangia upatikanaji wa sukari kijijini Magwamila na nchini kwa ujumla, pia watakamilisha yote yanayohitajika ili kuwezesha uzalishaji kamili wa sukari tani 79,200 kwa mwaka zitazalishwa katika awamu ya kwanza na awamu ya pili hadi kufikia kiasi cha 118,000 tani kwa mwaka.

**7.0 MUDA WA MAKUBALIANO**

Hivyo, Mkataba huu wa Makubaliano utaanza rasmi kutumika mara tu pande zote husika zitakaposaini, na utadumu kwa muda wa miaka kumi (10) kwa awamu ya kwanza. Kwa makubaliano ya Pande Zote mkataba huu utahuishwa kila baada ya miaka kumi (10) kulingana na mahitaji ya wakati huo.

**8.0 SHERIA ZA MAKUBALIANO YA MKATABA**

Mkataba huu wa Makubaliano utatambuliwa na kutafsiriwa kwa sheria za Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

**9.0 MGOGORO NA USULUHISHI**

Endapo kutatokea tofauti au mgogoro baina ya pande zote mbili za Mkataba huu, basi tofauti au mgogoro huo utatatuliwa kwa njia ya mazungumzo baina ya pande zote mbili, na endapo kama suluhu ya tofauti hiyo au mgogoro huo haitapatikana basi Msuluhishi ambaye ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma akisaidiana na Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Ruvuma watasuluhisha mgogoro huo, na endapo itashindikana katika hatua ya usuluhishi basi yeyote katika Mkataba huu asiye ridhika na maamuzi hayo anaweza kupeleka mgogoro huo katika Mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza jambo hilo kwa hatua zaidi za kisheria.



KSH

HALMASHAURI YA KIJIJI
REG: NO: KIJ. 313
MAGWAMILA

**UMETIWA** sahihi hapa **SONGEA** na **HALMASHAURI YA KIJIJI CHA MAGWAMILA**

Leo 23 Mwezi 01 Mwaka 2024

Sahihi/Muhuri

Jina KASSIM SAIDI MKUMBA
Anwani S.L.P 995 SONGEA
Saini
Cheo MWENYEKITI WA KIJIJI

Jina ALLY SAIDY HUMBARO
Anwani S.L.P 995 SONGEA
Saini
Cheo AFISA MTENDAJI WA KIJIJI

**UMETIWA** sahihi hapa **SONGEA** na **SONGEA SUKARI LIMITED**

Leo……. Mwezi…… Mwaka 2024

SONGEA SUKARI LIMITED
P. O. Box 2924
DAR-ES-SALAAM

Sahihi/Muhuri

Jina KAPIL JAYANTILAL DAVE
Anwani P.O.Box 9273, DSM
Saini
Cheo MWAKILISHI-SONGEA SUKARI LTD

Jina KUMAR KRISHNAN
Anwani P.O.Box 9273
Saini
Cheo MKURUGENZI-SONGEA SUKARI LTD